TANGAZO LA SERIKALI NA. 233 la tarehe 4/4/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),
SURA YA 287

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA KUZUIA NA KUDHIBITI SUMUKUVU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 791 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ngodo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Kuzuia na Kudhibiti Sumukuvu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ya Mwaka 2025, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya Kuzuia na Kudhibiti Sumukuvu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ya Mwaka 2024 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 13

2. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya kanuni ya 13 kama ifuatavyo:

"Wajibu wa mmiliki wa mazao

13. Mmiliki wa mazao anayesafirisha mazao kutoa shambani atahakikisha vifungashio anavyotumia kuhifadhia mazao wakati wa kusafirisha ni vikavu na visivyoruhusu maji, unyevu na vumbi kuingia ndani ili kuepusha kuvu kuota kwenye mazao".

Dodoma
12 Machi, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*